

**AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA AMRI YA MAREKEBISHO YA JEDWALI  
LA NNE LA SHERIA YA USHURU WA BIDHAA, SURA YA 147 (THE EXCISE  
(MANAGEMENT AND TARIFF) ACT, CAP. 147)**

---

**KWA KUWA**, Sheria ya Fedha ya mwaka 2011 (Na. 5 ya mwaka 2011) ilifanya marekebisho kwenye Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 kwa kuweka tozo ya ushuru wa bidhaa kwenye maji yanayohifadhiwa kwenye chupa kwa kiwango cha shilingi sitini na tisa kwa lita;

**NA KWA KUWA**, tathmini ya ushuru huo imebainisha kwamba tozo hiyo imeathiri ushindani wa bidhaa za maji yanayozalishwa hapa nchini na kuathiri uzalishaji wa bidhaa hii kwa viwanda vya ndani ya nchi;

**NA KWA KUWA**, kifungu kidogo cha (7) cha kifungu cha 124 cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 kinampa mamlaka Waziri wa Fedha, kwa kupitia Amri iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, kufanya marekebisho kwenye Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, kwa lengo la kupunguza au kuongeza viwango vya ushuru wa bidhaa zilizoainishwa katika Jedwali hilo;

**NA KWA KUWA**, kifungu kidogo cha (8) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 kinaelekeza kwamba marekebisho yatakayofanyika kwenye Jedwali la Nne, lazima kuridhiwa na Bunge kupitia Azimio la Bunge;

**NA KWA KUWA**, Waziri wa Fedha, kwa kuzingatia umuhimu wa kulinda viwanda vya ndani kutokana na ushindani na viwanda vya nje, na kwa lengo la kuongeza mapato na ajira kwa Watanzania na kwa kupitia Amri iliyotangazwa kwenye Tangazo la Serikali Na.332 la mwaka 2011, amefanya marekebisho kwenye Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya

147 kwa kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye maji yaliyohifadhiwa kwenye chupa kutoka shilingi sitini na tisa kwa lita hadi shilingi kumi na mbili kwa lita;

**HIVYO BASI**, kwa kuzingatia umuhimu wa marekebisho hayo, Bunge hili katika Mkutano wa Sita na kwa mujibu wa kifungu cha 124(8) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, sasa linaazimia kuridhia punguzo la ushuru wa bidhaa kutoka shilingi sitini na tisa na kuwa shilingi kumi na mbili kama Waziri wa Fedha alivyotangaza kupitia Tangazo la Serikali Na. 332 la mwaka 2011.

Dodoma,  
31 Januari, 2012

**MUSTAFA H. MKULO**  
*Waziri wa Fedha*